


JUA UKWELI KUHUSU CHANJO YA COVID-19

Chanjo hufundisha mwili wako kupambana na magonjwa.

Chanjo za COVID-19 huupa mwili wako maelekezo ya kujifunza jinsi virusi vya corona vinavyoonekana. Kisha mwili wako huvunja chanjo na kuiondoa. Ukipata virusi hivi baadaye, mwili wako unaweza kuvitambua na kuvishambulia mara moja. Una uwezekano mdogo wa kuugua sana kwa sababu mwili wako umeandaliwa.




Huwezi kupata COVID-19 kutokana na chanjo.

Chanjo hizo hazina virusi hai vya corona, kwa hivyo haziwezi kukupa ugonjwa huo. Baada ya kupata chanjo, unaweza kuhisi uchovu, kuumwa na mkono, au upate homa kwa siku moja au mbili. Hiyo ni kawaida—inamaanisha mwili wako unajenga ulinzi.

Chanjo ni nzuri sana katika kuzuia magonjwa hatari.

Ingawa chanjo haziwezi kukuzuia kuambukizwa, zinaweza kuokoa maisha yako. Watu wenye afya nzuri wa umri wowote wanaweza kupata dalili kali na za muda mrefu, na hatari kubwa zaidi ikiwa una unene kupita kiasi, kisukari, au shinikizo la damu. Watu wengi ambao wamelazwa hospitalini hivi karibuni kutokana na COVID-19 hawajapata chanjo. Na ikiwa tayari umekuwa na virusi, chanjo zinaweza kukusaidia ukiugua tena.



Chanjo za COVID-19 zimejaribiwa kwa makini kwa ajili ya usalama.

Maelfu ya wajitoleaji wa umri tofauti, rangi, makabila na jumuiya mbalimbali waliwasaidia watafiti kuhakikisha kuwa chanjo ni salama kwa kila mtu. Mamilioni zaidi kote ulimwenguni sasa wamepokea chanjo hizo kwa usalama. Unapopata chanjo, madaktari huangalia kwa karibu athari adimu, zisizotarajiwa. Hakuna ushahidi kwamba chanjo huathiri uwezo wako wa kupata watoto. Kwa ujumla, hatari za COVID-19 ni kubwa zaidi kuliko hatari za chanjo.

WAUGUZI WAKO HAPA KUKUSAIDIA!

NI SAWA KUWA
NA MASWALI
KUHUSU CHANJO
ZA COVID-19.



Children's Vaccine
EDUCATION PROJECT

